**HOTUBA YA MGENI RASMI BALOZI MHANDISI JOHN W. H. KIJAZI, KATIBU MKUU KIONGOZI KATIKA UFUNGUZI WA MAONESHO YA KIMATAIFA YA UTALII (*SWAHILI INTERNATIONAL TOURISM EXPO - S!TE 2019*) KATIKA UKUMBI WA MLIMANI CITY TAREHE 18 OKTOBA, 2019**

---

*Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii;*

*Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliohudhuria katika shughuli hii;*

*Mheshimiwa Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mheshimiwa Kemirembe Lwota (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii;*

*Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii;*

*Mheshimiwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam;*

*Mheshimiwa Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Utalii Tanzania;*

*Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Prof. Adolf Mkenda, Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii;*

*Bi. Devota Mdachi, Mkurugenzi Mwendeshaji, Bodi ya Utalii Tanzania;*

*Wawakilishi wa Mabalozi;*

*Wakuu wa Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama;*

*Washiriki wa Onesho la S!TE kutoka ndani na nje ya nchi;*

*Waandishi wa habari;*

*Wageni Waalikwa;*

*Mabibi na Mabwana;*

Habari ya asubuhi na karibuni sana katika maonesho haya ya Kimataifa ya Utalii ambayo ni maarufu kwa jina la *S!TE.*

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda nianze kwa kukushukuru, na kueleza furaha yangu kwa kupata fursa hii ya kutembelea na kufungua rasmi maonesho haya ya Kimataifa ya Utalii, yanayojulikana kama *Swahili International Tourism Expo - S!TE*.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alitamani sana kuja kufungua maonesho haya yeye mwenyewe, lakini kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayomkabili, Mheshimiwa Rais amenituma nije kufanya kazi hii ya kufungua maonesho haya kwa niaba yake. Mheshimiwa Waziri, wewe na Watumishi wote wa Wizara yako mnafahamu jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais anafuatilia kwa karibu sana juhudi zinazofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii, za kuvutia watalii wengi zaidi kuja kutembelea nchi yetu. Kwa jinsi ambavyo leo nimeshuhudia maonesho haya yalivyofana, sitasita kumfahamisha Mheshimiwa Rais kuhusu mambo mazuri niliyoyaona hapa, na kazi kubwa na nzuri ya kutangaza Utalii wa nchi yetu inayofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Utalii, Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yako na wadau wote wa utalii hapa nchini, ikiwa ni pamoja na mchango mkubwa unaotolewa na Sekta Binafsi. Kwa hakika maonesho haya ni kielelezo tosha cha ubunifu na jitihada mnazofanya ili kuiweka Tanzania katika hadhi yake inayostahili ya utalii duniani.

Napenda kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa uongozi wako ambao pia umewezesha maonesho haya kufana kwa kiwango kikubwa.

Kama ambavyo umeeleza, maonesho haya ya S!TE yamekuwa yakifanyika kila mwaka tokea mwaka 2014, kwa hiyo hii ni mara ya tano sasa kwa maonesho haya kufanyika chini ya uratibu wa Bodi ya Utalii Tanzania. Nimefahamishwa kwamba kila mwaka maonesho haya yamezidi kuwa bora. Hivyo, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Bodi ya Utalii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jaji Mstaafu Thomas MIHAYO, kwa uratibu mzuri wa Maonesho haya mwaka hadi mwaka.

***Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Kama tulivyojulishwa awali, maonesho ya S!TE ya mwaka huu yamehusisha wafanyabiashara wakubwa wa utalii takribani 400, na mawakala zaidi ya 200 wa Kimataifa kutoka nchi mbalimbali duniani. Kwa niaba ya Serikali, natoa shukrani zetu za dhati kwa washiriki wote, kwa kutenga muda wenu kuja kuungana nasi katika kutangaza utalii wa nchi yetu. Ni matumaini yetu kwamba wageni wote, hasa wale waliotoka nje ya nchi yetu, watafurahia ukaaji wao hapa nchini, na watakaporejea kwenye nchi zao watakuwa mabalozi wetu wa kuitangaza Tanzania duniani kote. Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wageni wetu wote waliokuja nchini kwa ajili ya kushiriki katika tukio hili muhimu wanaishi kwa usalama, amani na utulivu kwa muda wote watakaokuwepo hapa nchini.

***Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Tanzania tunafurahi kwamba, kasi ya kukua kwa sekta ya utalii wetu ni nzuri. Wakati mwaka jana (2018) utalii kwa nchi zote duniani ulikua kwa wastani

wa asilimia sita (6%), kwa upande wa Tanzania, utalii ulikua kwa asilimia kumi na tatu (13%), ambayo ni takriban mara mbili ya wastani wa ukuaji wa sekta hiyo duniani.  Kwa hiyo ni dhahiri kuwa Tanzania tunaendelea vizuri katika sekta ya Utalii.

Utalii ni kati ya Sekta zinazoongoza kwa kuingiza fedha nyingi za kigeni hapa nchini. Mwaka jana inakadiriwa kwamba utalii peke yake, umeingizia nchi yetu Dola za Kimarekani bilion 2.4, ambayo ni sawa na robo ya fedha zote za kigeni tulizopata mwaka jana. Kadhalika utalii unachangia asilimia kumi na saba na nusu (17.5%) ya pato la Taifa. Huu ni mchango mkubwa sana kwa uchumi wetu. Vilevile, sekta ya utalii inatoa ajira rasmi na zisizo rasmi kwa wananchi wetu. Hivyo, ni lazima tuendelee kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba sekta hii inabaki kuwa imara, na inazidi kukua.

Hata hivyo, pamoja na mchango mkubwa wa kiuchumi kutoka katika sekta ya utalii, na kasi nzuri ya ukuaji wake mwaka hadi mwaka, bado idadi ya watalii wanaoingia nchini Tanzania ni ndogo ukilinganisha na wingi na uzuri wa vivutio vyetu vya utalii. Kwa mfano, mwaka jana (2018) makisio yanaonesha kwamba jumla ya watalii milioni moja na nusu (1,500,000) waliingia nchini. Idadi hii siyo tofauti sana na idadi ya watalii wanaotembelea visiwa vya Mauritius. Ni wazi kwamba tunayo fursa kubwa sana ya kuongeza idadi ya watalii, na hivyo kufanya mchango wa sekta hii kwa uchumi wetu kuwa mkubwa zaidi.

Ndio maana Serikali ya Awamu ya Tano, inafanya juhudi kubwa katika kukuza sekta ya utalii. Juhudi hizi ni pamoja na kuimarisha miundombinu kama vile barabara, reli na viwanja vya ndege. Kadhalika, Serikali imelifufua Shirika letu la Taifa la ndege la “Air Tanzania” (ATCL) ili kuimarisha usafiri wa anga. Juhudi

kubwa pia zinafanyika kuimarisha mazingira ya biashara nchini, ili kuvutia wawekezaji wengi kwenye sekta mbali mbali, ikiwa ni pamoja na wawekezaji kwenye sekta ya utalii.

Tunatambua kwamba bila kuwa na sekta binafsi imara na iliyohamasika, hatutaweza kukuza uchumi wetu kwa kasi inayotakiwa. Hivyo, juhudi za Serikali za kuimarisha mazingira ya biashara, hasa kupitia kwenye utekelezaji wa Mwongozo wa Kuboresha Mazingira ya Biashara, maarufu kama '**Blueprint**', ni juhudi ambazo zitasaidia sana kukuza uchumi, ikiwa ni pamoja na kukuza sekta ya utalii. Ni dhahiri kuwa kwa namna ya pekee kabisa, sekta ya utalii inategemea sana mchango wa sekta binafsi, hasa kwenye ujenzi na uendeshaji wa mahoteli, na kwenye huduma za usafiri.

***Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Serikali pia inatambua umuhimu wa kukuza utalii kwenye maeneo yote hapa nchini. Kwa sasa hivi tunapata watalii wengi wanaotembelea Kaskazini mwa nchi yetu, ili kuona Mlima Kilimanjaro na kutembelea maeneo ya Ngorongoro, Serengeti, Tarangire, Manyara na Hifadhi ya Taifa ya Arusha. Bado tutaendelea kukuza utalii katika maeneo haya. Hata hivyo, kama kweli tunataka kuongeza utalii kwa kiwango kikubwa zaidi, ni lazima tufungue maeneo yote ya nchi yetu kwa ajili ya utalii, kwa sababu tunavyo vivutio vya kutosha katika mikoa yote ya nchi hii. Ndiyo maana Serikali imeanzisha mradi mkubwa wa "REGROW" kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, kwa ajili ya kukuza utalii katika eneo la Nyanda za Juu Kusini. Vilevile, Serikali imeanzisha hifadhi nyingine mpya za Taifa kutokana na mapori ya akiba ya Burigi, Kimisi, Biharamulo, Ibanda na Rumanyika, katika ukanda wa Kaskazini Magharibi mwa nchi, kwa minajili ya kutawanya fursa

za utalii nchi nzima. Pia, Serikali inakamilisha mchakato wa kutangaza hifadhi ya taifa ya Nyerere ambayo itakuwa kubwa kuliko zote Barani Afrika, na hifadhi nyingine mbili kutoka kwenye mapori ya akiba ya Ugalla na Moyowosi katika ukanda wa Magharibi mwa nchi.

Napenda kusisitiza kuwa ili tukuze utalii wetu, ni muhimu kwa Wizara husika, na Wadau wote kuendelea na jitihada za kutangaza vivutio vyote vya utalii (vipya na vya zamani) katika maeneo yote hapa nchini. Ni kwa sababu hiyo napenda kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Watumishi wote wa Wizara yako, kwa kushirikiana na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kufanya maonesho yaliyofana sana ya "Karibu Kusini" mnamo mwezi Septemba mwaka huu, na kuendesha jukwaa la uwekezaji kwenye sekta ya utalii, sambamba na maonesho hayo. Nawashukuru na kuwapongeza sana Wakuu wa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Songwe, Rukwa, Katavi na Morogoro, kwa kusimamia maonesho hayo ambayo mwaka huu yamefikia hadhi kubwa sana na kuvuta wadau wengi kutoka ndani na nje ya nchi yetu. Nafahamu kwamba Wizara yako, kwa kushirikiana na mikoa katika kanda nyingine, mnapanga kuendesha maonesho kama yale ya "Karibu Kusini" ili kutangaza vivutio vya kanda hizo. Endeleeni kuandaa maonesho hayo katika kanda nyingine kwa kushirikisha mikoa husika kikamilifu, na pia kwa kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi. Tengeni muda wa kutosha kufanya maandalizi ya maonesho hayo, ili yawe yenye ufanisi na tija inayotarajiwa.

***Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***;

Mkakati mwingine wa kukuza utalii ni kupitia kuongeza mazao ya utalii hapa nchini. Kwa sasa utalii wetu umejikita zaidi kwenye kutembelea mbuga za

wanyama. Hata hivyo, tunayo fursa kubwa ya kukuza **utalii wa fukwe, utalii wa kuvinjari kwa meli na utalii wa mikutano**. Haya ni maeneo mapya ambayo Serikali inayafanyia kazi kama mkakati mwingine wa kukuza utalii kwa kasi kubwa zaidi.

Ninafurahi pia kuona kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imeendeleza shughuli za Tamasha la Urithi, yaani *Urithi Festival*, mwaka huu. Matamasha haya ni kichocheo kingine cha kuongeza utalii nchini, kama tukiyaimarisha na kuzidi kuyaboresha kufikia viwango vya kimataifa. Mwaka huu matamasha ya Urithi yamekuwa mazuri zaidi, na yameongeza masuala muhimu, kama maonesho ya vinyago huko Mtwara, maonesho ya **mvinyo na ala za asili za muziki** huko Dodoma, mashindano ya **mieleka** na mashindano ya **kuimba kwaya** huko Mwanza na kadhalika. Tukiendelea hivi, mengi ya matamasha yetu haya yataingia kwenye kalenda za dunia za utalii, na hivyo kuongeza idadi ya watalii hapa nchini. Nafurahi kwamba matamasha haya yanaendeshwa kwa kushirikisha mikoa na wadau binafsi kikamilifu, na kwa kutumia wataalam kutoka sehemu mbali mbali, ikiwa ni pamoja na kutoka kwenye vyuo vyetu vikuu.

Hongereni sana Wizara husika, na wadau wote mnaohusika katika kufanikisha shughuli za Tamasha la Urithi.

***Mheshimiwa Waziri;***

Maonesho ya S!TE ni moja tu ya mambo mengi ambayo Serikali, kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na kupitia Bodi ya Utalii, inayafanya ili kutangaza utalii wetu. Juhudi kubwa pia zinafanyika kwa kutangaza utalii wetu nje ya nchi

kupitia ushiriki wa maonesho ya kimataifa kwenye nchi mbalimbali, na kupitia *road shows* zinazoandaliwa na Serikali yetu. Juhudi hizi zimeanza kuzaa matunda. Tunaona makundi ya watalii yakiongezeka kutoka nchi mbalimbali kutokana na juhudi hizi. Hivi karibuni tumepokea idadi kubwa ya watalii kutoka nchi ambazo awali hazikuwa zikileta watalii wengi. Watalii hawa ni kutoka China, Hong Kong, Israel, Malaysia na Korea. Kuna kila dalili kwamba tutafikia lengo letu la kupata watalii **milioni mbili** ifikapo mwaka 2020. Pamoja na pongezi nyingi ambazo Wizara na taasisi zake inastahili, napenda kuipongeza na kuishukuru sana sekta binafsi kwa umahiri wake wa kusaidia kutangaza utalii wetu, na kwa kutoa huduma nzuri ambayo imesaidia sana kututangaza vizuri kama nchi.

Natoa pia pongezi na shukrani kwa balozi zetu zote zilizo nje ya nchi kwa kufanya juhudi kubwa za kuvutia watalii kuja hapa nchini. Najua mabalozi wetu wamesaidia sana kufanikisha maonesho haya ya S!TE, hivyo nawashukuru pia na kuwapongeza sana.

Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba na kuwahimiza wadau wote kutembelea maonesho haya hapa Mlimani City. Kupitia maonesho haya, wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo, watapata fursa ya kuanzisha ushirikiano na ubia. Pia, wageni watakaotembelea maonesho haya watapata fursa ya kupata habari muhimu kuhusu utalii. Kwa hiyo ni vizuri kila atakayeweza asikose fursa hii, na aje kujionea mwenyewe jinsi maonesho haya yalivyofana.

***Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Nichukue nafasi hii pia kuihakikishia dunia kwamba Tanzania ni nchi salama kabisa. Tanzania ni nchi ya amani, na hakuna jambo lolote la kutishia

usalama, wala afya ya mtu yeyote anaetembelea nchi yetu. Serikali iko imara kabisa kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa salama na yenye amani.

Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kuelezea matumaini yangu kuwa, maonesho haya ya *Swahili International Tourism Expo* kwa mwaka huu wa 2019 yatakuwa yenye mafanikio makubwa kwenu ninyi wote mnaoshiriki. Aidha, nachukua fursa hii kuwatakia safari njema washiriki wote kutoka nje ya Tanzania, pindi mtakapokuwa mnarudi nchini kwenu. Nawashauri msiondoke bila ya kutembelea baadhi ya vivutio vyetu vya utalii, ikiwemo fukwe bora duniani katika visiwa maarufu vya Zanzibar na Mafia, hifadhi bora zaidi Afrika ya Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambalo ni eneo muhimu zaidi duniani, kwa historia ya uwepo wa binadamu wa kale duniani, pamoja na binadamu kuishi na wanyama, na maeneo mengine mengi ya kuvutia hapa nchini. Ni matumaini yetu pia kwamba, mwakani mtakuja tena kuungana nasi kwenye maonesho haya ya S!TE, na maonesho mengine ambayo Tanzania itayaandaa na kuwaalika.

Mheshimiwa Waziri pamoja na Washiriki wote, sasa napenda kuchukua nafasi hii kutamka rasmi kuwa, Maonesho haya ya *Swahili International Tourism Expo* 2019 yamefunguliwa rasmi.

**AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**